JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA

TANGAZO

UUZAJI WA MITI YA MISAJI KWA NJIA YA MAKUBALIANO BINAFSI (PRIVATE AGREEMENT) KATIKA SHAMBA LA MITI MTIBWA, MOROGORO NA LONGUZA, MUHEZA TANGA

TAREHE 07/03/2017

1. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) unatarajia kuuza miti aina ya Misaji yenye jumla ya meta za ujazo **10,800.420** iliyopo mashamba ya miti ya Mtibwa na Longuza yaliyopo mikoa ya Morogoro na Tanga mtawalia. Mauzo haya yatafanyika Machi 21, 2017 katika chuo cha Taifa cha Utalii Kampasi ya BUSTANI kilichopo katika makutano ya Mtaa wa Shaaban Robert/Samora Avenue mjini Dar es Salaam saa nne na nusu (4:30) asubuhi. Uuzaji huu utafanyika kwa njia ya makubaliano binafsi (private agreement) kwa kuzingatia kanuni 31 (iii) ya kanuni za sheria ya misitu za mwaka 2004. Miti hii ya misaji itauzwa mahali ilipo na jinsi ilivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo.

2. Kampuni au mtu binafsi anayetaka kushiriki mauzo kwa njia ya makubaliano binafsi anatakiwa kuwasilisha maombi kwenye bahasha iliyofungwa kuonesha nia ya kushiriki mauzo kwa njia ya makubaliano binafsi akiambatisha leseni ya biashara, Usajili wa kiwanda cha kuchakata magogo (2016/17), usajili wa biashara ya mazao ya Misitu (2016/2017) na cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN). Aidha, anatakiwa aoneshe jina la shamba, jina la kiunga, namba ya kitalu/vitalu na ujazo anaotarajia kununua kama ilivyo kwenye jedwali namba 1 na 2 hapo chini,

3. Baada ya kuwasilisha maombi hayo mnunuzi ataitwa kwenye majadiliano (negotiation) na Wakala wa Huduma za misitu Tanzania. Maafikiano yakifikiwa, mnunuzi ataelekezwa kufanya malipo kama inavyooneshwa katika kipengele Na. **9**. Baada ya malipo hayo mnunuzi ataingia mkataba wa kisheria wa manunuzi ya miti ya misaji kati yake na TFS.

4. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania unawaalika wanunuzi kutuma maombi yao kwa ajili ya kufanya majadiliano ya kununua miti ya misaji kwa njia ya makubaliano binafsi ambapo mnunuzi anaweza kuchagua viunga vifuatavyo;

JEDWALI Na. 1: KIUNGA NAMBA KH2B NA KH2C SHAMBA LA MITI LONGUZA

Na.	Jina la Kitalu	Ujazo kwa kitalu (m^3)	Bei ya awali/kitalu/m^3
1	KH 2B-PA04	403.620	750,000
2	KH 2B-PA06	401.404	750,000
3	KH 2B-PA08	452.352	750,000
4	KH 2B-KW 1	741.714	750,000
5	KH 2B-KW 2	243.000	750,000
6	KH 2B-KW 3	303.593	900,000
7	KH 2B-KW 4	307.872	900,000
8	KH 2C-01	549.727	900,000
9	KH 2C-02	663.417	900,000
10	KH 2C-03	597.021	900,000
11	KH 2C-04	641.215	900,000
12	KH 2C-05	201.759	900,000
Jumla ya ujazo		**5,506.690**	

JEDWALI Na. 2: KIUNGA NAMBA MT 11 SHAMBA LA MITI MTIBWA

Na.	Jina la kitalu	Ujazo wa kitalu (m^3)	Bei ya awali/kitalu/m^3
1	MT 11- C8	400.05	
2	MT 11-D1	344.366	700,000
3	MT 11- D2	415.078	700,000
4	MT 11- D3	397.646	700,000
5	MT 11- D4	300.512	700,000
6	MT 11- D5	203.485	700,000
7	MT 11- D6	203.876	700,000
8	MT 11- D7	301.206	700,000
9	MT 11- D8	200.162	700,000
10	MT 11- D9	203.434	700,000
11	MT11-T1	201.434	700,000
12	MT11-T2	200.000	700,000
13	MT11-T3	301.064	700,000
14	MT11-T4	200.052	700,000
15	MT11-T5	201.271	700,000
16	MT11-T6	214.993	700,000
17	MT11-T7	218.993	700,000
18	MT11-T8	159.277	700,000
19	MT11-J1	300.201	700,000
20	MT11-J2	326.625	700,000
Jumla ya Ujazo		**5,293.725**	

5. Mnunuzi atakayefanikiwa kununua miti ya misaji hataruhusiwa kusafiirisha magogo nje ya nchi kwa mujibu wa kanuni ya 50(1) ya mwaka 2004. Kusafirisha Mazao ya Misitu nje ya nchi ni baada ya kuyachakata kwa Mujibu wa Tangazo la Serikali Na 69 la mwaka 2006.

6. Makampuni na watu binafsi wanakaribishwa kutembelea viunga shambani wakati wa saa za kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:00) alasiri isipokuwa siku za sikukuu. Meneja wa shamba au msaidizi wake atakuwepo kwa ajili ya maelekezo zaidi.

7. Wanunuzi wanapaswa kuchukua na kusoma masharti ya uvunaji kwa kila shamba. Masharti hayo yanapatikana ofisi za shamba husika.

8. Bei ya kianzio kwa mita moja ya ujazo imeoneshwa katika Jedwali namba 1 na 2 hapo juu ikijumuisha 'VAT', 'CESS' na 'LMDA'.

9. Mnunuzi atakayeshinda atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani yote ya mazao ya misitu aliyonunua siku tatu (3) baada ya makubaliano kufanyika. Fedha hizo hazitarudishwa iwapo mnunuzi ataghairi. Asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki italipwa ndani ya miezi miwili baada ya kusaini mkataba wa mauziano na Wakala. Malipo yatafanyika katika Akaunti ya shamba la Miti husika kama inavoonekana hapa chini;

i. SHAMBA LA MITI MTIBWA,	**ii. SHAMBA LA MITI LONGUZA,**
AKAUNTI NA. 22010000567	**AKAUNTI NA. 41901000015**
NMB – TURIANI	**NMB – MUHEZA**

10. Mnunuzi atapaswa kuwasilisha hati ya malipo (pay – in – slip) ya benki kwa meneja wa shamba kama uthibitisho wa malipo si zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.

11. Mteja atatakiwa kuondoa mazao ya misitu aliyonunua ndani ya miezi miwili baada ya kumaliza kulipa malipo yote kwa asilimia 100.

12. Tangazo hili pia linapatikana katika tovoti zifuatazo za Wakala na Wizara: www.tfs.go.tz, na www.mnrt.go.tz

13. Maombi yote yawasilishwe siku ya mauzo kabla ya saa 4:00 asubuhi. wanunuzi watakaochelewa kuwasilisha maombi yao kwa siku na muda uliopangwa hawataruhusiwa kushiriki katika majadiliano ya mauzo.

limetolewa na

MTENDAJI MKUU

S.L.B 40832,

DAR ES SALAAM.